

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

Telegrams “AFYA”, **DODOMA**
Nambari ya simu: **255-026-2323267/2351196**
Fax Na.255-22-2138060
(Barua zote ziandikwe kwa **Katibu Mkuu**)



Mji wa Serikali-Mtumba,
Barabara ya Afya,
S.L.P 743,
40478 DODOMA.

**UFAFANUZI KUHUSU TAARIFA YA UPOTOSHAJI ILIYOCAPISHWA NA
GAZETI LA NIPASHE LEO JUMAMOSI TAREHE 18 FEBRUARI, 2023**

DODOMA: FEBRUARI 18, 2023

Gazeti la Nipashe lenye usajili wa ISSN 0856. Na. 0581225, lililotolewa leo siku ya jumamosi, tarehe 18 Februari, 2023, limechapisha habari ukurasa wake wa kwanza na wa pili kuwa **“Wagonjwa wapewa dawa zilizokwisha muda wa matumizi”**.

Baada ya kupitia habari hiyo kwa kina, tumegundua kwamba hakuna sehemu yoyote ilioandikwa kuwa wagonjwa wanapewa dawa zilizoisha muda wake wa matumizi kama ilivyoandikwa na gazeti hilo.

Uongozi wa Wizara ya Afya umesikitishwa sana na upotoshaji huu uliochapishwa kwa makusudi, wenyewe lengo la kuleta tataruki katika jamii na kurudisha nyuma juhudzi za Serikali za utoaji huduma bora nchini.

Wizara ya Afya inatambua uwepo wa dawa zilizoisha muda wake katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya dawa katika matibabu, mathalani mabadiliko katika ARV na vitendanishi vya kupima UKIMWI kuelekea dawa na vitendanishi bora zaidi. Serikali ina utaratibu wa kuzitenga, kuzitunza na kuziteketeza dawa hizi ikiwa ni pamoja na kuwahusisha wadau kugharamia uteketezaji wake. Ifahamike kuwa uwepo wa dawa hizo haumanishi wanapewa wagonjwa.

Uongozi wa Wizara ya Afya unalitaka Gazeti la Nipashe kuomba radhi kutokana na upotoshaji huu na kuchapisha kwa uzito uleule kama ambavyo wamefanya katika chapisho lao la leo tarehe 18 Februari, 2023.

Wizara ya Afya inatoa wito kwa Wakurugenzi wa Hospitali zote, Waganga Wakuu Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa na Wilaya kuhakikisha wanakamilisha taratibu za kuomba vibali ili kuteketeza dawa zilizoisha muda wake.

Imetolewa na;

A handwritten signature in blue ink, appearing to read "Aminiel Buberwa Aligaesha".

Aminiel Buberwa Aligaesha

**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
WIZARA YA AFYA**